WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA, BIASHARA NDOGO SANA, NDOGO NA ZA WASTANI, UVUMBUZI NA MASHIRIKA

# CHATA YA UTOAJI HUDUMA YA WANANCHI

**RUWAZA**
Kuwa mwezeshaji wa ushindani na uwekezaji endelevu, biashara na ukuaji wa viwanda katika Kaunti ya Kitui

**WITO**
Kuendesha uwekezaji jumuishi kwa kukuza biashara, uwezeshaji wa biashara ndogo sana, ndogo na za wastani, na mashirika na kukuza uvumbuzi kwa maendeleo endelevu.

**MAADILI YA KIMSINGI**
- Uongozwaji na Mteja
- Uwajibikaji
- Ujumuishaji
- Uwazi
- Utaalam
- Ufaafu na Ufanisi
- Ushirikiano Adilifu
- Haki na Usawa

| Nbr | Huduma/ Bidhaa | Mahitaji ya Kupata Huduma / Bidhaa | Gharama ya Huduma/ Bidhaa (Ikiwa Ipo) | Makataa |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Uthibitisho na upigaji muhuri wa vifaa vya upimaji | Uwasilishaji wa vifaa kwa ukaguzi, kujaribiwa na kupigwa muhuri | Sh. 50 hadi Sh 3,500 kulingana na ukubwa na aina | Ziara zilizoratibiwa na zenye utaratibu katika makaazi ya mfanyabiashara kwa ukaguzi na uthibitisho wa upimaji wa vifaa ndani ya dakika 20 |
| 2. | Uthibitisho na upigaji muhuri wa vifaa vya upimaji | | Sh. 50 hadi sh 2,400 kulingana na ukubwa na umbo | |
| 3. | Ukaguzi wa kabla ya bidhaa kupakiwa na uchunguzaji wa matendo ya kibiashara yasiyo ya haki | Usampulishaji na kuangaliwa kwa uzani kwa bidhaa kabla ya kupakiwa kutafanywa katika makaazi ya mwanabiashara | Sifuri | Usampulishaji wa bidhaa kabla ya kupakiwa ndani ya dakika 30 |
| 4. | Habari kuhusu nafasi za uwekezaji | Inapoombwa | Sifuri | Ndani ya siku 1. Habari sanifu kupatikana kwa urahisi. |
| | | Kama sehemu ya huduma za ziada | Sifuri | Utaratibu na papo hapo. |
| 5. | Kusajiliwa kwa mashirika ya kijamii | Ufunzaji kabla ya mashirika, kuundwa kwa sheria ndogo, fomu za ombi zilizojazwa na uwasilishaji wa hati za lazima | Sifuri | Ndani ya siku 7 baada ya notisi |
| | | Kupelekwa kwa hati kwa msajili na kupokewa kwa cheti | Sh. 3,700 | Takriban ndani ya siku 14 baada ya hati zote kuwasilishwa |
| 6. | Kuhudhuria mikutano ya kijumla ya mashirika ya kijamii | Notisi inapopokewa | Sifuri | Kimwaka |
| 7. | Ukaguzi wa mashirika | Ombi linapofanywa na uwasilishali wa akaunti za kifedha | Inatofautiana | Kimwaka |
| 8. | Kushughulikia na kutekeleza mahitaji yote ya uchapishaji na utangazaji kwa kaunti | Ombi linapofanywa/ utambuzi unapohitajika | Sifuri | Kukamilishwa ndani ya siku 14 baada ya kuidhinishwa kwa mchakato wa ununuzi |
| 9. | Kushiriki katika shughuli za Kaunti za uchapishaji na utangazaji k.v makongamano na maonyesho ya kibiashara | Utambuzi unapohitajika/ kwa ombi | Sifuri | Ndani ya siku 7 kutegemea sura ya tukio |
| 10. | Huduma za mikopo za bei nafuu | Utoaji wa fomu za kuomba mkopo na uchunguzi wa fomu za mkopo zilizojazwa kikamilifu | Sifuri | Ndani ya siku 21 |
| | | Bodi kukubali na mkopo kutolewa | Sifuri | Ndani ya siku 28 |
| 11. | Kufunzwa kwa makundi | Ombi la kibinafsi au kulingana na ratiba iliyopangwa | Sifuri | Ndani ya siku 14 hitaji linapoanzishwa. |

**VIWANGO VYA HUDUMA ZETU**

**Wateja wetu watashughulikiwa kwa njia ya kitaalam na adabu.**
**Simu zitapokewa kila wakati na baruapepe zitajibiwa katika saa rasmi za ufanyakazi za 8:00 asubuhi hadi 5:00 jioni.**

**NAMNA YA KUFANYA MALALAMISHI**

**Panapowezekana, tutakabiliana na malalamishi mara moja. Ikiwa hujatosheka na majibu yetu, utatuma malalamishi yako kirasmi kwa kuandikia:**

**Mwanakamati mtendaji wa Kaunti,**
**Wizara ya Biashara, Viwanda, Biashara Ndogo Sana,**
**Ndogo na za Wastani, Uvumbuzi na Mashirika**
**S.L.P. 33-90200, Kitui**
**Simu: 0746 219 340 | 0741 291 737**
**Barua Pepe: trade@kitui.go.ke**

**AU**

**Ofisa Mkuu Mtendaji (Ombudsman)**
**Tume ya Kiutawala ya Haki (CAJ)**
**West End Towers, Ghorofa ya 2**
**S.L.P. 20414 - 00200 Nairobi**
**Simu: 254 20 227 00 00 | Kupiga Bila Malipo: 0800 221 349**
**www.ombudsman.go.ke**

*Rasilimali Zetu, Uwekezaji Poa, Maisha Poa*